



6 February 2018

## Siku ya Usalama Mtandaoni 2018

### C-Sema kuungana mkono na mashirika mbalimbali duniani kuadhimisha Siku ya Usalama Mtandaoni 2018

**Leo (Jumane 6 Februari, 2018) shirika la C-Sema** linashiriki katika na kampeni ya Siku ya Usalama Mtandaoni ili kuhamasisha matumizi salama ya teknolojia na yenye ufanisi.

Maadhimisho ya Siku ya Usalama Mtandaoni yanaratibiwa Uingereza na Kituo cha Usalama Mtandaoni cha Uingereza (UK Safer Internet Centre). Kauli mbiu ya mwaka huu ni "Tengeneza na sambaza maudhui yenye heshima: Mtandao salama unaanza na wewe"

Siku hii huadhimishwa na nchi zaidi ya 100 duniani na mwaka huu C-Sema itaungana na mashirika mbalimbali kutoka Uingereza na duniani kote ili kuhamasisha jamii ijenge mtandao ulio salama na bora hasa kwa matumizi ya watoto.

Katika kusherehekea siku hii, shirika la C-Sema limekuwa likitoa elimu kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii juu ya matumizi sahihi na salama ya Intaneti kwa watoto na kujenga uelewa kuhusu tovuti ya kutoa taarifa za picha na video zipatikanazo mtandaoni zenye maudhui ya unyanyasaji wa kingono kwa watoto iliozinduliwa Oktoba mwaka jana.

Will Gardner, Mkurugenzi wa Kituo cha Usalama Mtandaoni, Uingereza (UK Safer Internet Centre) na Mkurugenzi Mtendaji wa Childnet, alisema:

"Siku ya Usalama Mtandaoni ni fursa kwa kila mtu nchini Uingereza na duniani kote kushirikiana ili kuhakikisha uwepo wa mtandao bora na salama. Ikiwa wewe ni kijana, mzazi, mlezi, shule au shirika, sote tunaweza kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha mtandao ni mahali salama. Shule nyingi na mashirika mbalimbali yameahidi kushiriki katika kuadhimisha siku hii muhimu na ushirikiano huu unasaidia kuhakikisha siku hii inaleta matokeo chanya, kwa kuwafikia 42% ya watoto wa Uingereza mwaka 2017 na kufikia idadi kubwa zaidi ya watoto kila mwaka."

**Thelma Dhaje, Meneja wa Kituo cha Huduma ya Simu Kwa Mtoto Tanzania Bara, alisema:** "Tunafurahia kuwa sehemu ya siku hii ambayo inahamasisha mtandao salama na bora kwa watoto wetu na jamii kwa ujumla. Siku hii itakuwa na mchango katika usalama wa mtandao Tanzania ambao unakua kwa kasi. Vilevile, itatusaidia kuwapa watoto ujuzi wa matumizi sahihi na salama ya mtandao na kuwalinda wakiwa mtandaoni. "

Soma zaidi kupitia: [www.saferinternetday.org.uk](http://www.saferinternetday.org.uk).

Tovuti ya kutoa taarifa kuhusu picha na video za unyanyasaji wa kingono kwa watoto: <https://report.iwf.org.uk/tz>